



**SOCIETAS DIVINI SALVATORIS
CURIA GENERALIZIA DEI SALVATORIANI**

Ufficio Roma 47 - Casella Postale 102
Via della Conciliazione, 51
00193 ROMA (Italia)

Pd. Milton Zonta SDS
Mkuu wa Shirika

Itifaki Na. AVB – 120 - SWA

Roma, 19 juni 2020

Kwenu ndugu wote wa Familia ya Kisalvatorian

Yah: Tangazo la Muujiza

Wapendwa Wanafamilia ya Kisalvatorian,

Kwa furaha kubwa tunapenda kuwatangazia kuwa Baba Mtakatifu, Papa Francis, katika halaiki kubwa ya watu siku ya 19 juni 2020 amepokea hati ya muujiza toka kwa Mwadhama Kardinali Angelo Becciu, Mkuu wa Idara ya Kutakatifuza Watu, na kuidhinisha Idara hiyo hiyo kutangaza muujiza uliohusishwa na maombezi ya Mwanzishi wetu, Mstahiki Mtumishi wa Mungu, Padre Francis Maria wa Msalaba Jordan.

Hatua hii imemaliza mchakato wa muujiza na dhahiri kufungua njia katika kutangazwa Mwenyekheri mpendwa Mwanzishi wetu. Mara tu tarehe na mahali pa sherehe ya kutangazwa mwenyekheri itakapoamuliwa na Vatikano tutawatangazia.

Ningependa niwaalike tuendelee kusali kupitia maombezi ya Padre Francis Jordan na kujitayarisha mtu mmoja mmoja na kama jumuiya kwa tukio hili la maana sana kidini na kiroho tulilolisubiri kwa muda mrefu ili liweze kututia moyo sisi sote katika kuwa waaminifu kwa Karama yetu ya Kisalvatorian.

Ninayeungana nanyi kwa moyo wote na katika sala.

Milton Zonta, SDS

Pd. Milton Zonta sds
Mkuu wa Shirika



G. Agustín Van Baelen

Pd. Agustín Van Baelen sds
Katibu Mkuu